

Mkate wa Siku

SIKU
31

NENO LA SIKU | Mei, 2022

SIKU 01 - 2 SAMUELI 22:33 (SUV)

"Mungu ndiye ngome yangu yenye nguvu; Naye huwaongoza wakamilifu katika njia yake."

SIKU 02 - ISAYA 58:11a (BHN)

"Mimi Mwenyezi-Mungu nitawaongozeni daima, nitatosheleza mahitaji yenu wakati wa shida."

SIKU 03 - ZABURI 119:49 (ONEN)

"Kumbuka neno lako kwa mtumishi wako, kwa sababu umenipa tumaini."

SIKU 04 - WARUMI 8:14 (NEN)

"Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio watoto wa Mungu."

SIKU 05 - DANIELI 2:20 (SUV)

"Danieli akajibu, akasema, Na lihimidiwe jina la Mungu milele na milele; kwa kuwa hekima na uweza ni wake."

SIKU 06 - WAEBRANIA 10:22a (BHN)

"na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tumeoshwa miili kwa maji safi."

SIKU 07 - KUMB. 33:12b (ONEN)

"Yuamfunika mchana kutwa, Naye hukaa kati ya mabega yake."

SIKU 08 - NEHEMIA 9:31b (SUV)

"...kwa maana wewe u Mungu mwenye neema, mwenye rehema."

SIKU 09 - 2 WAKORINTHO 4:7 (BHN)

"Basi, sisi tulio na hazina hiil tuko tu kama vyombo vya udongo, m ili ionekane wazi kwamba nguvu hiyo kuu yatoka kwa Mungu wala si kwetu sisi wenyewe."

SIKU 10 - MATHAYO 9:29b (NEN)

"...Na iwe kwenu kama mnavyoamini."

SIKU 11 - ISAYA 26:3 (ONEN)

"Utamlinda katika amani kamilifu yeye ambaye moyo wake ni thabiti kwa sababu anakutumaini wewe."

SIKU 12 - EZEKIELI 36:9a (SUV)

"Maana, tazama, mimi nasimama upande wenu, nami nitawaelekea."

SIKU 13 - KUMBUKUMBU 28:8 (BHN)

"Baraka za Mwenyezi-Mungu zitakuwa katika ghala zenu za nafaka na katika shughuli zenu zote."

SIKU 14 - ISAYA 44:2a (NEN)

"Hili ndilo asemalo Bwana, yeye aliyekuhuluku, aliyekumba tumboni, yeye atakayekusaidia..."

SIKU 15 - WAFILIPU 4:4 (ONEN)

"Furahini katika Bwana siku zote, tena nasema furahini."

SIKU 16 - YOHANA 14:27a (SRUV)

"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo."

SIKU 17 - KUTOKA 15:6a (SUV)

"BWANA, mkono wako wa kuume umepata fahari ya uwezo."

SIKU 18 - MATHAYO 5:5 (BHN)

"Heri walio wapole, maana hao watairithi nchi."

ENDELEA UKURASA UNAOFUATA...

SIKU 19 - 1 PETRO 5:6 (SUV)

"Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake;"

SIKU 20 - 2 WAKORINTHO 6:2a (RSUV)

"Kwa maana asema, Kwa wakati uliokubalika nilikusikia, Na katika siku ya wokovu nilikusaidia;..."

SIKU 21 - ZABURI 62:8 (BHN)

"Enyi watu, mtumainieni Mungu daima; mfungulieni Bwana yaliyo moyoni mwenu. Mungu ndiye kimbilio la usalama wetu."

SIKU 22 - EZRA 8:22b (NEN)

"Mkono wa neema wa Mungu wetu uko juu ya kila mmoja anayemtafuta, lakini hasira yake kubwa ni dhidi ya wote wamwachao."

SIKU 23 - ISAYA 26:12 (ONEN)

"Bwana, unaamuru amani kwa ajili yetu, yale yote tuliyoweza kuyakamilisha ni wewe uliyetenda kwa ajili yetu."

SIKU 24 - EZEKIELI 34:26b (RSUV)

"nami nitaleta manyunyu kwa wakati wake; yatakuwako manyunyu ya baraka."

SIKU 25 - YOELI 2:21b (SUV)

"kwa kuwa BWANA ametenda mambo makuu!"

SIKU 26 - YEREMIA 1:19b (BHN)

"maana mimi nipo pamoja nawe, asema BWANA, ili nikuokoe."

SIKU 27 - YOHANA 16:24b (NEN)

"Ombeni nanyi mtapewa, ili furaha yenu ipate kuwa kamili."

SIKU 28 - ZABURI 4:8 (RSUV)

Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara, Maana Wewe, BWANA, peke yako, Ndiwe unijaliaye kukaa salama.

SIKU 29 - UFUNUO 1:8 (BHN)

"Mimi ni Alfa na Omega," asema Bwana Mungu Mwenye Nguvu, aliyeko, aliyekuwako na anayekuja

SIKU 30 - ISAYA 49:16a (SUV)

"Tazama, nimekuchora katika vitanga vya mikono yangu..."

SIKU 31 - ZABURI 111:9 (RSUV)

"Amewapelekea watu wake ukombozi, Aameamuru agano lake liwe la milele, Jina lake ni takatifu na la kuogopwa.!"

**Makala hii imechukuliwa
kutoka
www.biblesociety.ca © Haki
zote zimeifadhiwa.**

*Tunawashukuru sana kwa kuungana
na sisi kueneza Neno la Mungu hapa
Tanzania na duniani kote kwa ujumla.*

Chama cha Biblia cha Tanzania
16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>
<https://tanzanian.bible/>
<https://biblesociety-tanzania.org>



&



**Canadian
Bible Society**

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA